


## SEHEMU ZA NCHI NA MIKOA NDANI YA NORWAY



Nchi ya Norway imegawanywa katika sehemu tano. Kaskazini mwa Norway (**Nord-Norge**) iko mbali ya Kaskazini .

Katikati ya nchi inapatikana **Trøndelag**.

Magharibi inapatikana Vestlandet na mashariki Østlandet. Sehemu ya nchi iliyopo kusini ya mbali inaitwa Sørlandet.

Kila sehemu ya nchi imegawanyika katika mikoa. Kuna mikoa 11 ndani ya Norway.

### Kaskazini mwa Norway

#### (Nord-Norge)

Sehemu ya kaskazini mwa Norway inapatikana kwa kuelekea kaskazini na mashariki.

Eneo hili linapatikana mikoa miwili, Troms na Finnmark na Nordland.

Kama utakuja Norway- kaskazini (Nord-Norge) mwezi Desemba ama Januari, unaweza kushuhudia kipindi cha giza. Kunakuwa na Kipindi cha giza wakati juu linakuwa chini ya mstari wa horizonto.



Nordlys. Foto: Pxhere.com

Kipindi cha kiangazi unaweza kushuhudia juu la usiku wa manane. Jua la usiku wa manane ni wakati ambapo jua hali zami, na sehemu ya jua ipo juu ya mstari wa horizonto kwa siku nzima.

## Troms na Finnmark

Troms na Finnmark iko mbali kuelekea kaskazini na mashariki mwa Norway, na kuna mipaka ya nchi ya Urusi, Finland na Sweden. Tromsø ni mji mkubwa ndani ya Troms na Finnmark. Pointi iliyoko kaskazini zaidi ya Norway ni Knivskjelodden, inapatikana ndani ya Troms na Finnmark. Sehemu inayojulikana zaidi ni Nordkapp inayopatikana karibia sawasawa umbali wa kaskazini kama Knivskjelodden. Nordkapp ni sehemu maarufu kwa watalii.



Nordkapp Foto: Andrey Armyagov, AdobeStock

Hammerfest, ni jiji lilopo kaskazini zaidi duniani, linapatikana ndani ya Troms na Finnmark.

## Nordland - Kaskazini mwa Norway

ni mkoa mrefu na mwembamba uliopaka na nchi ya Sweden. Bodø ndio mji mkubwa zaidi ndani ya Nordland.



Skrei henger til tørk på hjell. Kilde: Nærings og fiskeridepartementet

Lofoten ipo katika Nordland na ina visiwa vingi sana. Kutoka Januari mpaka Aprili, shughuli za uvuvi zinafanyika ndani ya Lofoten. Katika uvuvi eneo la lofoten wanapatikana samaki aina ya **Skrei** kwa wingi. **Skrei** ni aina ya **Cod** ambao hukaa kaskazini ya mbali katika bahari ya barens. Kutoka Januari hadi Aprili huogelea **skrei** hadi Lofoten kutaga mayai. Sehemu kubwa ya **cod** wanaokamatwa hukaushwa. Samaki hao huitwa samaki wa kukaushwa. Sehemu kubwa ya samaki waliokaushwa husafirishwa nje ya nchi kama vile Italia na Nigeria.

Mzunguko wa arktiki (**polarsirkelen**) unapita Nordland. Kaskazini mwa mzunguko wa arktiki (**polarsirkelen**) kuna kipindi cha giza na juu la usiku wa manane. Jinsi unavyozidi kwenda kaskazini zaidi, ndivyo siku zenye kipindi cha giza na juu la usiku wa manane zinazidi kuwepo. Nordkapp kuna kipindi cha giza kuanzia 20

Novemba hadi 22 Januari, na juu la usiku wa manane kuanzia 14 Mei hadi 29 julai.

## Trøndelag

Trøndelag inapatikana katikati ya nchi na ni eneo/sehemu na mkoa. Sehemu hii pia huitwa katikati ya Norway (**Midt-Norge**).

Trøndelag ina **fjord** ndefu na mlima mrefu.

Trollhetta ndio mlima mrefu. Trøndelag imepakana na nchi ya Sweden.

Jiji kubwa ndani ya Trøndelag ni Trondheim. Trondheim ni jiji la tatu kwa ukubwa nchini Norway. Nidarosdomen ni kanisa kuu ndani ya Trøndelag. Kanisa lilijengwa juu ya kaburi la mtaktifu Olav.

Mtakatifu Olav alikuwa Viking. Aliishi kwenye miaka ya mwaka 1000. Alifika katika nchi nyingine za ulaya na alisikia kuhusu ukristo. Na hapo ndipo akaahidi ukristo ndio itakuwa dini itakayo ruhusiwa nchini Norway. Kanisa la Nidarosdomen linapatikana Trondheim



Nidarosdomen Kilde: Pixabay.com

Røros ni jiji linalopatikana ndani ya Trøndelag. Mji wa Røros unapatikana juu ya milima ya Røros. Jiji lilijengwa huko kwa

sababu iligundulika madini ya shaba kwenye mlima mnamo mwaka 1644. Kukatengenezwa machimbo ya madini ya shaba. Watu wakahamia Røros kwa ajili ya kupata kazi kwenye migodi. Na hivyo ndivyo jiji la Røros likakua.



Røros Foto: Lars Geithe, Flickr

## Mashariki mwa Norway (Østlandet)

Østlandet ni sehemu ya nchi yenye mikoa mingei. Mikoa katika mashariki ya nchi ni Oslo, Vestfold na Telemark, Viken na Innlandet. Østlandet ni sehemu/eneo lenye utajiri wa watu ndani ya Norway ikiwa na wakazi zaidi ya 2.5 milioni. Hii ina maanisha nusu ya wakazi wa Norway wanaishi mashariki mwa Norway (Østlandet).

Glomma ni mto mrefu zaidi Norway. Glomma una urefu wa 619 kilomita na unatiririka kuanzia Trønelag huko kaskazini

## Landsdeler og fylker i Norge – Kiswahili

mpaka kusini Østlandet na una tokea  
Fredrikstad.



*Glomma har sitt utløp i Fredrikstad. Kilde: Wikipedia*

Mlima mrefu Norway unapatikana  
Østlandet. Galdhøpiggen ni mlima mrefu  
Norway. Una urefu wa mita 2469. Hii ina  
maana kilele cha Galdhøpiggen kipo mita  
2469 toka usawa wa bahari.



*Galdhøpiggen. Kilde:Wikimedia Commons*



*1Mjøsa. Kilde: Wikipedia*

## Oslo

Oslo ni mji mkuu Norway na jiji kubwa  
zaidi Norway. Oslo ni mkoa na iko sehemu

ya ndani ya Oslo **fjord**. Jumba la mfalme,  
bunge na serikali zipo Oslo.



*Stortinget Foto: Sergii Figurmyi, Adobestock*

## Vestfold na Telemark

Vestfold na Telemark ni mkoa unao anzia  
eneo la pwani na kuelekea juu ya milima.

Mlima mrefu zaidi katika Vestfold na  
Telemark ni Gaustadtopenn.

Gaustadtopenn upo ndani ya Rjukan na  
una urefu wa mita 1883 kutoka usawa wa  
bahari.



*Gaustadtopenn. Nede i dalen ser vi Rjukan by. Foto:  
Eystein M. Andersen, Riksantikvaren, Flickr*

Maji ya Farris yako ndani ya Vestfold na  
Telemark. Maji yenye madini yaitwayo  
Farris yamepewa jina toka maji ya Farris.  
Lakini Farris hayatoki katika maji ya Farris,

wana kinga kutoka chanzo ndani ya msitu  
Bøkeskogen katika eneo lililo karibu.



Bøkeskogen i Larvik Foto: Jostein, Adobestock

Tønsberg iko ndani ya vestfold na Telemark na ni mji mkongwe Norway. Mji huu ulianzishwa karibia katika mwaka 870. Ngome ya mlimani (*Slottsfjellet*) iko ndani ya Tønsberg na ni mji wa makumbusho ya kale na ni mkubwa zaidi kaskazini mwa Ulaya.



Slottsfjellet i Tønsberg Foto: Celine, Adobestock

## Viken

Viken ni mkoa wenye utajiri zaidi wa watu Norway. Mkoa umepakana na Sweden. Viken inasambaa kuanzia Oslo fjord juu mpaka kwenye milima, kutoka mpakani

mwa Sweden na mpaka katikati ya kusini mwa Norway.

Miji mikubwa ni Drammen, Lillestrøm na Fredrikstad.

## Ndani ya nchi (Innlandet)

Ndani ya nchi (**Innlandet**) ni mkoa ambaa hauna pwani. Mkoa unapakana na nchi ya Sweden. Mto mkubwa zaidi Norway ni Mjøsa. Mjøsa uko ndani ya mkoa wa ndani ya nchi (**Innlandet**). Mjøsa inajulikana kwa kuwa na meli iitwayo Skibladner. Skibladner ni meli kongwe zaidi nchini Norway inayoendelea kufanya kazi. Skibladner ina safari kati ya Eidsvoll, Hamar, Lillehammer na Gjøvik.



Skibladner er et dampskip. Foto: Mahlum, Riksantikvaren

## Kusini mwa Norway (**Sørlandet**)

Kuna mkoa mmoja tu ndani ya kusini mwa Norway (**Sørlandet**), unaoitwa Agder. Sørlandet ina **skjærgård** yenye visiwa, na sehemu nyingi za kuogelea.



*Skjærgård Kilde: Flickr.com*

Mji mikubwa wa kusini mwa Norway (**Sørlandet**) ni Kristiansand. Bustani kubwa ya wanyama Norway ipo Kristiansand, inaitwa bustani ya wanyama (**dyrepark**) ya Kristiansand, lakini watu wana penda kuita kwa kifupi “Bustani ya wanyama”(**Dyreparken**)



*Lemurer i Kristiansand dyrepark. Foto: Kommunal – og - moderniseringsdepartementet*

## Magharibi mwa Norway (**Vestlandet**)

Mikoa ndani ya magharibi mwa Norway (**Vestlandet**) ni Møre na Romsdal, Vestland na Rogaland. Magharibi mwa Norway (Vestlandet) ina julikana duniani kwa kuwa na **fjord** ndefu na milima mirefu. **Fjord** ndefu Norway, iitwayo

Sognefjorden iko ndani ya magharibi mwa Norway (**Vestlandet**). Ina urefu wa kilomita 204.



*Balestrand ligger ved Sognefjorden Foto: mariusltu, Adobestock*

Karibu miji yote ya magharibi mwa Norway (Vestlandet) iko kwenye pwani. Miji mikubwa katika sehemu hii ya nchi ni Bergen, Stavanger, Ålesund na Haugesund.

## Rogaland

Jiji kubwa ndani ya Rogaland ni Stavanger. Waligundua mafuta katika bahari ya kaskazini (**Nordsjøen**) mwishoni mwa miaka ya 1960. Ika amuliwa ofisi kuu za viwanda vya mafuta viwepo ndani ya Stavanger. Kulikuwa na wafanyakazi wanane hapo mwanzoni. Mmoja wapo

alitoka nchini Iraki na jina lake ni Farouk Al-Kasim.



Oljeplattform Foto: Wikipedia

## Magharibi mwa Norway (Vestland)

Jiji kubwa ndani ya mkoa wa magharibi mwa Norway (Vestland) ni Bergen. Bergen ni jiji la pili kwa ukubwa Norway, mara nyingi huitwa pia makao makuu ya magharibi mwa Norway (Vestlandets). Bryggen ni eneo linalojulikana na maarufu ndani ya Bergen.



Bryggen i Bergen Foto: Michelle Maria, Pixabay

Kuna barafu iliyoganda isiyoyeyuka (**isbreer**) nyingi nchini Norway. Barafu iliyoganda isiyoyeyuka (**isbreer**) ni eneo kubwa lenye barafu. Maeneo mengine kuna baridi kipindi cha kiangazi na

kusababisha theruji kuto yayuka. Na hivyo kuna kuwa na theruji nyingi kila mwaka. Na dheruji inakuwa barafu. Wakati eneo lenye barafu linapozidi kuwa kubwa na zito lina anza kuteremka chini ya mlima, na kuwa barafu iliyoganda isiyoyeyuka (**isbreer**).

Barafu iliyoganda isiyoyeyuka (**isbreer**) kubwa nchini Norway inaitwa Jostedalsbreen. Jostedalsbreen iko katika mkoa wa magharibi mwa Norway (**Vestland**).



Jostedalsbreen Foto: Tania Zbrodko, Adobestock



## Landsdeler og fylker i Norge – Kiswahili

Sehemu/eneo tambarare juu ya mlima .  
Miti haioti katika eneo hili bali kunakuwa  
na vichaka tu.

Hardangervidda ni eneo kubwa zaidi na  
tambarare juu ya mlima ndani ya Norway.  
Ipo katika mikoa ya Vestland, Viken na  
Vestfold na Telemark.




*Hardangervidda Foto: By-studio, Adobestock*

## Møre na Romsdal


Jiji kubwa ndani ya Møre na Romsdal ni  
Ålesund, Molde na Kristiansund.

Maporomoko ya maji marefu zaidi Norway  
yapo Møre na Romsdal, yanaitwa  
Vinnufossen. Maporomoko maarufu zaidi  
ni Vøringsfossen, yapo mkao wa  
mwagharihi mwa Norway (Vestland).  
Hakuna maji mengi sana katika  
maporomoko ya maji marefu zaidi  
Norway.



*Figur 3Vinnufossen. Foto: Carl S Bj, Wikipedia*

Midsundtrappen ni ngazi za mawe zenye  
ngazi 2200. Zilijengwa na wajenzi toka  
Nepali.



*Steintrapp Foto: Arild, Adobestock*